*Kioo cha Lugha, Juz. 23(2), 206-233*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i2.6

# Motifu ya Utumwa na Utabaka ndani ya Kisiwa cha Pate: *Utendi wa Mwanakupona* kama Tarihi ya Kihistoria

*Tom Olali*[1]

## Ikisiri

*Utendi wa Mwanakupona* ni utenzi uliotungwa na mwanamke, Mwanakupona binti Mshamu Nabhany, kumnasihi bintiye Mwana Hashima bint Shee Mataka na kumshauri namna ya kuwa mke mwema kwa mumewe. Mwanakupona alikuwa binti wa Mshamu Nabhany na mkewe Mohammed Is-Haq Mbarak. Alizaliwa mjini Pate mwaka 1810 (Senkoro, 2011). Awali *Utendi wa Mwanakupona* ulitungwa kwa hati za Kiarabu. Katika fasihi ya Kiswahili, kazi ya kihistoria ya *Uhuru wa Watumwa* (1934) iliyotungwa na James Mbotela ndiyo maarufu na inaangazia motifu ya watumwa. Hata hivyo, kuna kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili kuhusu utumwa. Wapo wahakiki wengine ambao wanauangalia *Utendi wa Mwanakupona* kama utumwa wa kimawazo au utumwa wa ukandamizaji wa wanawake. Makala imechunguza motifu ya utumwa na utabaka katika Kisiwa cha Pate kilichoko kaunti ya Lamu. Mazungumzo ya kikundi lengwa yalishirikisha baadhi ya wakazi wa kisiwa cha Pate na maeneo ya Lamu ambao waliulizwa mitazamo yao kuhusu mada husika na kutoa fursa ya kubadilishana mawazo na wengine ambao walikuwa na maoni tofauti. Tulisikiliza, kuandika madokezo, na pia kurekodi mazungumzo katika mazingira yao ili kupata taarifa za moja kwa moja kuhusu mada ya utafiti. Vilevile, uchanganuzi wa data ya pili ulifanyika katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

## 1.0 Utangulizi: Utumwa na Utabaka katika Fasihi

Dhana ya utendi[2] ina fasili mbalimbali kulingana na wataalamu tofautitofauti. Utendi una sifa kuu ya urefu, huwa na beti nyingi sana, aghalabu hufikia mamia hata maelfu, zinazosimulia au kuzungumzia masuala mbalimbali kama vile ya kidini, kishujaa, kimapenzi, kihistoria au kiwosia. Mathalani, *Utendi wa Mwanakupona* unasimulia mawaidha ya mama kwa mawanawe wa kike na pia *Utendi wa*

[1] Profesa, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya,
Barua Pepe: tom.mboya@uonbi.ac.ke

[2] Pia, huitwa utenzi. Katika makala hii, tunarejelea “utendi”. Istilahi hizi mbili, “tenzi” na “tendi” hutumiwa kama visawe.

*Siiraji*[3] unaosimulia mawaidha ya baba kwa mwanawe wa kiume, Helewa, wenye beti 209. Kuna tendi zilizotungwa zinazosimulia waadhi, hususani *Utendi wa Mwanakupona*, *Utenzi wa Hati*[4], *Utenzi wa Siiraji*[5], *Utenzi wa Howani Mwana Howani*[6], na *Utenzi wa Adili*[7].

Kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu *Utendi wa Mwanakupona*, zikiwamo tafiti za Strobel (1979), Njozi (1990), Khatib (1985), Biersteker (1991), Swaleh (1992), Gibbe (1995) na Wandera (1996). Tafiti za baadaye ambazo zimechambua *Utenzi wa Mwanakupona* ni pamoja na Mulokozi (1999), Momanyi (2007), Beja na Mwinyifaki (2013), Timammy na Swaleh (2013), Munyole (2017) na Mulokozi (1983, 1996).

Mulokozi (1983, 1996) anaelezea utendi kuwa ni ushairi wa matendo. Ni utungo mrefu wenye kusimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Matukio haya huweza kuwa ya kihistoria lakini tendi nyingi huchanganya historia, visakale na hata visasili mlemle. Wamitila (2003) anasema kuwa utendi huelezea shairi refu la masimulizi kwa mapana linalohusu matendo ya mashujaa. Utendi unahusisha hadithi za kishujaa, visasili na hata chimbuko la taifa fulani. Wamitila anaendelea kubainisha aina mbili za utendi kuwa kuna utendi simulizi na vilevile utendi andishi. Finegan (2008) anapambanua utendi kuwa lazima uwe na urefu japo hajabainisha urefu wenyewe unafaa uwe wa kiasi gani kimishororo, beti na mizani. Vilevile, anaongezea kuwa unaweza kuwa na visa tofautitofauti ila viwe vinahusiana. Maelezo ya Wamitila, Mulokozi na Finegan kuhusu fasili ya dhana ya utendi yanashabihiana sana maana wote wanasema kuwa utendi ni ushairi. Wote wanadai kuwa ushairi wenyewe hujikita kwenye masuala ya kishujaa na simulizi za historia ya mtu au jamii.

*Utendi wa Mwanakupona* una karibu vigezo vyote vya kuufanya ufuzu kuitwa hivyo. Hivyo basi, ni sahihi kusema kuwa utendi ni utungo ambao huzungumzia masuala marefu ya kihistoria na mashujaa. Sifa nyingine madhubuti ya utendi ni kuzungumzia jambo au suala kwa kina au kwa undani kwani kwa kawaida utendi huwa na beti zaidi ya ishirini, kwa mfano, *Utendi wa Hamziyyah* una beti 446 na *Utumbuizo wa Liyongo Harusini* ni beti 36. Mifano ya tendi maarufu za Kiswahili ni kama vile: *Utendi wa Hamziyyah*[8], *Utendi wa Mwanakupona*,

---

[3] Mengi huhusu *Utendi wa Siiraji,* rejelea, Ngunjiri, Dadson (2012) *Matumizi ya Taswira kama Kigezo cha Kufanikisha Maudhui katika Utendi wa Siiraji uliyotungwa na Muhammadi Kijumwa*. Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

[4] Uliandikwa na Shabaan Robert mnano mwaka wa 1967.

[5] Uliandikwa na Muhammad Kijumwa.

[6] Ulitungwa na Zaynab Himid Mohammed, mzaliwa wa Malindi katika kisiwa cha Zanzibar.

[7] Uliandikwa na Shabaan Robert.

[8] Mengi zaidi kuhusu *Hamziyyah*, tazama Olali, T. (2004). *The Veneration of the Prophet: The Role of Kasida ya Hamziyyah during the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago,*

*Utendi wa Kasida, Ayi Wangi Wangi, Utendi wa Fumo Liyongo, Utendi wa Al-Inkishafi, Utendi wa Shufaka, Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na *Utendi wa Burudai.*

Wapo waandishi kama vile Radburn (2016), Stephen (2025), Nwulia (1975), Frederick (2023) ambao wamechunguza motifu ya utumwa. Radburn (2016) anachunguza utumwa akilenga hasa utumwa wa bahari ya Atlantiki kati ya 1640-1808 na wakati huohuo akiunganisha safari za wafanyabiashara wa Atlantiki na wale wa Afrika Mashariki. Anataja maeneo kama vile Caribbean, Jamaica, Barbados na Carolina ya Kusini. Anaendelea kuzungumzia utabaka ambapo Waingereza ndio walikuwa wahusika wakuu katika biashara hii. Kwa upande mwingine, Rockel (2025) anachunguza utumwa na utabaka katika masoko ya utumwa yaliyoko Afrika Mashariki. Anatoa sababu ya biashara hiyo kusambaa kwa jinsi ambavyo watumwa walitakiwa kukidhi mahitaji ya viwanda katika mataifa ya Magharibi. Anataja ukulima wa karafuu na masultani wa Omani waliokuwa kwenye tabaka la juu. Nwulia (1975) anajadili kwa undani utumwa wa Afrika Mashariki na walioshiriki walikuwa Waingereza, Waarabu na baadhi ya Waafrika ambao walikuwa kama makuadi wa soko huria. Kiriama (2018) kwa upande wake, anataja vituo na mastakimu na namna maeneo haya yalivyoathiri biashara ya utumwa. Anataja vituo ambavyo waliishi walowezi, barabara za biashara za utumwa, makazi ambayo watumwa walioachiliwa huru walikoishi. Makala yake yanatupa picha kamili ya jinsi wale walioishi katika maeneo mbalimbali walipopita watumwa walivyofasiri hali hizo.

## 2.0 *Utendi wa Mwanakupona*

Huu ni utendi mashuhuri uliotungwa na mwanamke kwa jina Mwanakupona binti Mshamu Nabhany. Mwanakupona alitunga utendi huu kwa matilaba ya kumnasihi bintiye Mwana Hashima bint Shee Mataka, kumshauri na kumpa wosia yeye pamoja na kina dada wenzake wa enzi hizo namna ya kuwa mke mwema kwa mumewe. Mwanakupona alikuwa binti ya Mshamu Nabhany na mkewe Mohammed Is-Haq Mbarak. Alizaliwa mjini Pate mwaka 1810 (Senkoro, 2011). *Utendi wa Mwanakupona* ulisambazwa kwa masimulizi na kuna baadhi ya miswada ambayo ni mirefu na mingine ni mifupi kufuatana na kumbukumbu za moyoni za wapokezi na wasambazaji (Senkoro, 1988). *Utendi wa Mwanakupona* mwanzo ulitungwa kwenye hati za Kiarabu. Baadaye ulitafsiriwa kwa Kiswahili kwa lahaja ya Kiamu na baadaye kwenye lugha ya Kirumi, hati rahisi kusomwa kwa wasomi wa kisasa (Hitchens, 1934). Yumkini Mwanakupona alitamalakia Lamu kutoka Siu ambako ndiko aliweza kuutunga utendi huu mnamo mwaka 1858. Bwana Shee Mataka alikuwa mtawala wa Siu na alipigana vita vya msituni kwa kipindi cha miaka ishirini akipinga utawala wa sultani wa Zanzibar, Seyyid Said. *Utendi wa Mwanakupona*

*Kenya*. Tasnifu ya PhD, SOAS, University of London (Imechapishwa).

una beti 102. Una urari wa vina, mizani nane katika kila mshororo. Utenzi huu unaangazia masuala ya kijamii kama vile ndoa na unyumba, dini na utabaka.

## 3.0 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, Utumwa na Utabaka

Makala imeongozwa na nadharia inayoakisi masuala ya kike katika jamii. Nadharia tunayoirejelea hapa ni ya Ufeministi wa Kiafrika. Nadharia hii imeangazia kwa kina masuala kuhusiana na maonevu ya mwanamke katika jamii. Maonevu yanayolengwa na nadharia hii ni pamoja na ndoa na kudunishwa katika kutoa maamuzi, kudhalilishwa na kuwekwa katika kiwango sawa na watoto, miongoni mwa dhuluma nyingine. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni nadharia iliyonyambuliwa abayo asili yake ni Nadharia ya Ufeministi. Nadharia hii ya Ufeministi ilichambuliwa na Mary Wollstonecraft mwaka 1792 huko Uingereza. Malengo ya mwandishi huyu yalikuwa kuonesha dhahiri mambo anayoyapitia mwanamke katika jamii. Baadaye, Mary Eagleton pamoja na Ross Murfin (1991) wakiwa kama baadhi ya wahakiki wa Nadharia ya Ufeministi walijizatiti kuainisha ufeministi katika matapo kwa kutumia maeneo na itikadi. Kiitikadi, walipata ufeministi huru, unaopigania haki za kibinadamu wa kijamaa. Ufeministi huru hutetea usawa wa wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha yao na ule wa kiharakati unaonesha uadui uliopo ndani ya mwanamume dhidi ya mwanamke na, hivyo, kuendelea kumdhalilisha mwanamke. Wa mwisho ni ufeministi wa kijamaa ambao unahimiza wanaume kushiriki katika majukumu ambayo huachiwa wanawake kama vile ya kulea watoto.

Makala hii imetumia Nadharia ya Ufeminsti wa Kiafrika na inashughulikia masuala ya wanawake na sifa zake zinaakisi tajiriba na hali halisi ya mwanamke wa Kiafrika. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika iliibuka mwanzoni mwa karne ya 20 na iliasisiwa kwa mtazamo wa mwanamke wa Kiafrika. Mmoja wa waasisi wake ni Olufemi Taiwo (1996). Yeye pamoja na waasisi wengine wa nadharia hii walikuwa na mtazamo sawa juu ya masuala ya wanawake barani Afrika. Mtazamo wa nadharia hii ni kuwa katika bara la Afrika, mwanamke wa Kiafrika hudhulumiwa na mfumo wa ubabedume ulilotiliwa nguvu na tamaduni na mila za jamii na ukawa umekita mizizi barani Afrika. Kutokana na hayo, wanaharakati wa masuala ya mtazamo kike barani Afrika waliendelea na ari za kumpigania mwanamke popote alipo. Wito wa kutaka kupigania haki na usawa ulitokana na msimamo wa baadhi ya wanasaikolojia waliomchanganua mwanamke na kumpa nembo mbalimbali kulingana na mtazamo wao.

Uana ni dhana inayodhihirisha majukumu ambayo ni ya kike na kiume. Hili lilizua mushkili maana majukumu aliyopewa mwanamke yalishahibiana na maumbile yake kama vile kuzaa, kulea, kupika na kadhalika. Majukumu haya yaliunda nafasi nzuri ya kumdunisha mwanamke na kuinua taasubi ya kiume, kuwa mwanamume huwa mbele na mwanamke ni wa kufuata mwanamume. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha mwanamke akubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kuikubali hali hiyo, mwanamke hufanywa chombo cha kuendeleza

utamaduni huo. Kwa ufupi ni kwamba, mtu hazaliwi mwanamke bali ni yale majukumu anayopewa kulingana na uana yanayomfanya mwanamke. Hivyo, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika haina budi kuzama katika mila, desturi na kaida za kijamii ili ibainishe nafasi ya mwanamke na uwezo wake katika utendakazi sambamba na anavyofanya mwanamume ili kubaini dhuluma atendewazo mwanamke.

Kwa namna inavyosawiri masuala ya jamii ya sasa, nadharia hii imetufaa katika kuweka wazi masuala ya utamaduni yanayomkandamiza mwanamke. Pia, inatuongoza kudhibiti mikakati ambayo mwanamke wa kisasa ameitumia kujimudu dhidi ya ubabedume ambao umekuwa sugu katika ufanisi wake kulingana na ulimwengu ulivyo. Yanayoangaziwa na nadharia hii ni pamoja na mahusiano ya jamii baina ya mwanamume na mwanamke, asasi za jamii zilizojengwa na kuhimiliwa kwa misingi ya uana, utamaduni wa kigeni na athari zake na maonevu mengine kama vile kudunishwa.

**4.0 Dhana ya Umwinyi na Utumwa Kisiwani Pate**

Kisiwani Pate[9], utawala ulikuwa wa kimwinyi[10]. Hata leo, kuna mitaa ya juu (Mitayuu) na mitaa ya chini. *Utendi wa Mwanakupona* umefinyangwa katika mastakimu ya umwinyi. Mfumo wa umwinyi ulisheheni katika funguvisiwa la Lamu, kikiwamo kile cha Pate. Katika mfumo huu wa utawala wa umwinyi, kitu kinachojitokeza dhahiri ni utabaka, ubaguzi na watu wanawekwa kwa madaraja ya juu na chini. Lile tabaka la juu kabisa linalotawala ndilo tabaka la mamwinyi na huwa wanamiliki nyenzo zote za uzalishaji na kumiliki mashamba *madal basari* na nyanja zote za kiuchumi. Senkoro (1988: 12-26) akimnukuu Mulokozi katika makala yake ya "Ushairi wa Kiswahili ni nini" anasema;

> Uozo na ubaradhuli wa maisha ya Kimwinyi hasa wakati mfumo huu unapoanza kutetereka kutokana na nguvu za jamii na za uchumi, huwafanya mamwinyi, katika maisha yao ya kizembe na kifasiki wapendelee sana mambo ya kuvutia macho na kuliwaza pia kama vile mapambo aina aina, wanawake wazuri, nakshi na marembo ya rangi za kuvutia katika makazi yao, marashi, manukato, udi, ubani na kadhalika.

Kisiwani Pate, vyombo vya pambo la wanawake vimesambaa kama vile ambari, furungu, bangili, vigome, vikuku, vibambaa, keekee, majasi, vipini, makungu na kadhalika. Maua na manukato yanazingatiwa kama vile viluwa, makoja, liwa, malangilangi, makumbura, behedani, zabadi, wanja na nargisi.

---

[9] Pate ni kisiwa kikubwa cha funguvisiwa la Lamu.

[10] Ni tofauti na ukabaila, unaotokana na neno la Kiarabu, *muqabil*, kurejelea mtu aliyezaliwa kutoka ukoo maarufu. Ni mfumo ule wa uchumi ambapo kabaila anamiliki mashamba na majumba na wapangaji wanalipa kodi.

Senkoro (1988) anasema kuwa maisha ya namna hii hujitokeza katika fasihi itokanayo na mfumo huu na motifu ya utumwa ilitokana na mfumo huu katika kipindi hiki cha umwinyi. Utawala wa Omani (1730-1890) katika upwa wa Afrika Mashariki ulikwenda unyounyo na mivutano, makabiliano, migogoro ya kisiasa ambayo matokeo yake yalikuwa kuibuka kwa baadhi ya tendi za kupinga utawala wa kisultani kama vile tungo za Muyaka bin Haji (k.1776-1840). Pia, kulikuwa na ustawi wa tabaka la juu la watawala wenyeji na Waarabu lililoiga mambo mengi ya utamaduni wa Kiarabu na kusisitiza kuzingatia mafundisho ya kidini. Hili nalo ni suala la kutatiza kwa maana utamaduni haujatenganisha mazuri na mabaya. Ni kile ambacho husemwa na wengi kuwa "kiingiacho mjini si haramu". Majilio ya Waarabu katika eneo la Afrika Mashariki yalileta dini ya Kiislamu na athari yake, tamaduni na mbeko za Uarabuni. Athari hizi zilipenya katika nyanja zote za maisha kama vile kielimu, kiuchumi, kiutawala, kiutamaduni, kisiasa na hata kidini. Baadhi ya Waafrika walisilimu na kuteuliwa kuwa viongozi na maimamu wa dini ya Kiislamu. Katika *Utendi wa Mwanakupona*, bintiye alipata wosia aliopewa uliohusiana na utamaduni wa kigeni. Tabaka hili lililokuwa na wasomi wengi lilitunga tenzi za kidini kama vile *Utendi wa Ras l'Ghuli*.

Makala yetu inajikita katika tapo la kwanza linaloongozwa na Senkoro (1988) ambapo anatoa mtazamo wake kuhusiana na *Utendi wa Mwanakupona*. Anajenga hoja zake kwa msingi wa utawala wa Kimwinyi ambao ulikuwa katika ukanda wa pwani ya Afrika ya Mashariki. Mamwinyi walipenda kuliwazwa. Kwa mujibu wa Senkoro (1988), mwanamke wa kipindi hiki alidhalilishwa na utawala na hali halisi ya Umwinyi. Anadai *Utendi wa Mwanakupona* uliendeleza utawala wa kimwinyi na utawala wa kidume. Kulingana na masuala nyeti yanayoibuka katika ulimwengu wa utandawazi, ni dhahiri kuwa wanawake walikuwa watumwa.

Ingawa utendi huu umeandikwa katika enzi za kimwinyi, watafiti wamelipa kisogo suala la utumwa pasipo kujua kuwa utumwa ulishamiri katika kisiwa cha Pate. Suala la ubabedume linajitokeza waziwazi katika *Utendi wa Mwanakupona*. Hii ni hali ambapo mwanamke hana haki mbele za mume, maamuzi yake hutupiliwa mbali na hivyo huishi kulingana na jinsi mwanamume alivyopanga. Kama ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika, kisiwani Pate, jamii ilikuwa ni ya kuumeni na ni jamii ambayo ilimpembeza mwanamke na kumweka katika ngazi ya chini. Upembezwaji wa mwanamke ulienea kote. Kwa muktadha huo, Mwanamke huwa hana uhuru wa kujiamulia na kujitawala. Kwa mwanamume, mwanamke ni kiumbe duni wa kuongozwa kulingana na maamuzi ya mwanamume. Mwishowe, mwanamke hukosa uhuru kabisa na huishia katika hali ya kunyanyaswa na mwanamume huyo. Huu ndio ubabedume na umekuwapo tangu jadi. Prins (1961) anazitaja koo saba za milki ya Pate kulingana na tabaka kutoka tabaka la juu la Nabahani hadi lile la chini kabisa la Wapate au Waswahili kama ifuatavyo:

i. Nabahani
ii. Masherifu
iii. Ozi (au al-Bauri)

iv. Hatimi
v. Abdi Salami
vi. Mafazii
vii. Wapate au Waswahili

**4.1 Kisiwa cha Pate na Umwinyi**

Kisiwa cha Pate kilichoko kaunti ya Lamu kina makabila yanayojulikana kama Wapate, Wasiyu, Watikuu na Washanga; na wote wana lahaja zao tofauti. Katika kisiwa cha Lamu, wapo Waamu, Wamatondoni, Wakipungani na Washela. Hawa wanazungumza lahaja moja ambayo ni Kiamu. Pia, wakazi wa Witu, Mkunumbi, Kipini, Mambrui na Malindi wanazungumza lahaja ya Kiamu. Olali (2004) anasema kuwa funguvisiwa la Lamu linapatikana kaskazini mwa pwani ya Kenya na linahusisha visiwa vitatu vikuu ambavyo ni Lamu, Manda na Pate na visiwa vingine vidogo kama vile Ndao (ndau) na Kiwayuu. Visiwa vya Lamu viliwekwa chini ya utawala wa Waarabu wa Omani katika karne ya 19 (Ylvisaker, 1975).

Olali (2004) anaelezea muundo wa wakazi wa Pate kitabaka. Anasema kuwa wapo wakazi wa kijiji kidogo *Mitayuu* na wale wa kijiji kikubwa, *Kitokwe* wanaosemekana ni watu wa asili ya nje. Kuna tofauti za kitabaka hadi leo kati ya watu wa *mtaa wa juu* na wale wa *mtaa wa chini*. Wale wa *mtaa wa juu* wanachukua majukumu makuu na mazito ya kijamii na pia wana uwezo mkubwa kiuchumi na kisiasa. Hata wakati wa kuikangaya[11], *Kasida ya Hamziyyah* wakati wa sherehe za Maulidi, washiriki wengi hutoka *mitaa ya juu* (Mitayuu).

Ili kufika Pate, unashukia Ras Mtangawanda. Kwa mujibu wa Olali (2004: 68), mji wa Pate ulijengwa katika karne ya 8. Katika karne ya 13, familia ya Nabahani ilikuwa watawala na katika karne ya 14 walianza kuvivamia visiwa vingine na, kwa njia hiyo, visiwa vyote vya Lamu vilikuwa chini ya himaya yao. Anaendelea kusema kuwa jamaa ya Nabahani wametamalakia Mombasa, Lamu, Unguja, Visiwa vya Komoro, Lindi, Mtwara na Bukini.

Pate ulikuwa ni mji mkuu na wa kutajika katika karne ya 17 na 18. Historia ya mji wa Pate inapatikana kwenye *Tarihi ya Pate*[12] na inasimulia jinsi ambavyo ilikuwa mahali muhimu hasa katika karne ya 14 wakati utawala wa Nabahani ulipoweka utawala wake hapo (Ghaidan, 1975). Anaendelea kusema kuwa, kwa wakati huu, utawala wa Pate ulikuwa ukishikilia sehemu kubwa kati ya Benadir upande wa kaskazini na Songo Mnara upande wa kusini. Utafiti uliofanywa na Chittick kuhusu *Tarihi ya Pate,* historia ya machimbo, inasema kwamba Pate haikustawi kabla ya karne ya 16 (Olali, 2004). Kwa Mujibu wa Chittick, utawala wa

[11] Kuhusu jinsi *Kasida ya Hamziyyah* inavyokangaiywa wakati wa sherehe za Maulidi kisiwani Lamu, tazama Olali, T. (2004).

[12] Marina Tomalcheva alihariri na kutafsiri miswada 177, 321, 344 na 358 inayopatikana katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, alitoa upya miswada ya C.H. Stigand, Alice Werner, M. Heepe na Alfred Voeltzkow.

Nabahani kisiwani Pate unakisiwa kuwapo katika karne ya 17. Tolmacheva (1993) anasema kuwa kulingana na simulizi katika *Tarihi ya Pate*, kulikuwa na mtawala mwenye asili ya Kiarabu kutoka familia ya Nabahani kule Oman ambaye alikuja Pate katika mwaka 600 A.H./1203-1204 B.K. Pia, katika simulizi nyingine inaelezwa kuwa msingi wa mji wa Pate na mingine unaenda nyuma hadi utawala wa Milki ya khalifa Umayyad, wakati Abd al-Malik bin Marwan (685-705) yumkini aliwatuma makundi ya Waarabu ambao walianzisha miji mingine thelathini na miwili. Viongozi waliofuata walikuwa na cheo cha usultani kando ya majina yao (Olali, 2012). Palikuwa vilevile na sultani mwanamke kwa jina Mwana Khadija (Tomalcheva 1993). Grenville anaelekea kukubalina na Tomalcheva anaposema kwamba, "Kulikuwa na jumla ya viongozi thelathini na watano, ambapo mmoja, alikuwa Mwana Khadija, mwanamke" (1988:).

Tomalcheva (1993) anatoa mfano wa Bwana Mkuu bin Muhammad (aliyefariki 973 A.H./1565-66 B.K) na kufuatiwa na Bwana Bakari bin Bwana Mkuu. Kwa mujibu wa Tomalcheva, mtu wa kwanza kutamalakia Pate kutoka familia ya Nabahani alikuwa Sulayman bin Sulayman Muzaffar al-Nabahani na wadogo zake wawili, wanaume, Ali bin Sulayman na Uthman bin Sulayman. "Na huyu Sulayaman bin Sulayman tuliyemtaja, yeye ndiye alikuwa sultani kule Arabia. Kisha alipata uongozi al-Yarubu na kwa hivyo akaja Pate, katika mwaka wa mia sita Hijra" (Tomalcheva, 1993). Olali (2004) anaeleza kuwa wakazi wa Pate wenyewe wana kumbukumbu ya baadhi ya watu muhimu ambao waliishi Pate. Wanawataja watu kumi kama vile Bwana Kitini (kutoka familia ya kimwinyi ya Nabahani), Abdul Malik bin Muriani (mwanzilishi wa miji ya pwani), Bakiumbe (kibaraka wa Manda), Mwana Inadhi (kiongozi wa Kitau huko Manda), na Suleyman (kiongozi wa kwanza wa Pate). Wengine walikuwa Ishaq (chifu wa Pate), Mwana Sukari binti Kai (dadake Sultani Fumoluti), Sheikh Abubakr bin Salim (mzee wa Pate), Sheikh Abubakr Mkanda (mtu mtakatifu) na hatimaye, Bwana Mtiti (nduguye Sultani Fumomadi). *Kitāb al-Zunūj*[13] cha karne ya 19 kinadai kuwa Khalifa Abd al-Malik bin Marwan (685-705) ambaye pia anajulikana kama Abdul Malik bin Muriani aliwatuma washamu kutamalakia pwani chini ya Amir Musa (Grenville, 1988).

Pate ulikuwa mji ambao una nguvu sana kwa karne nyingi. Pia, kulikuwa na hali kama ya utumwa huko na wakazi wa Pate wanakumbuka msemo: *Mwenda Pate Kauya, Kiuyacho ni kiriro* (Prins, 1961). Hii ina maana kwamba hakuna anayeingia Pate na kurudi salama na kwamba kinachorudi ni kilio. Hii inaonesha jinsi ambavyo watawala walitumia nguvu nyingi kuwadhalilisha watu na sifa ya utumwa. Msemo huu unarejelea Pate ambayo ilikuwa na nguvu za kisiasa na kiuchumi na kwamba waliweza kuwadhalilisha na kuwatesa majirani zao na kuchukua hata miswada yao

[13] Kwa Kiingereza ni *Book of the Zanj* na ni mswada wa kitabu uliomulika athari za Uarabu na imani ya Kiislamu miongoni mwa Waswahili. Unaeleza laana ya Ham, mwaka wa ndovu, unasimulia kabila la Kushur (Wamijikenda) walioishi Shungwaya mkabala wa mto Juba, kuwasili kwa Vasco da Gama na kifo cha Sultani Barghash bin Said wa Unguja.

(Olali, 2012). Kufikia karne ya 16, Pate ilikuwa mahali ambapo wasomi walipatikana na tendi maarufu kama vile *Hamziyyah*, *al-Inkishafi* na *Utendi wa Mwanakupona* zilipatikana (Olali, 2004: 71).

Mji wa Pate ulianza kuanguka baada ya kushindwa vita vikali kule Shela dhidi ya Wareno mnamo 1812. *Al-Inkishafi*, utendi ulioandikwa Pate katika kipindi hicho hicho, uliomboleza kuanguka kwake na enzi zake uliponawiri kama inavyoonekana katika ubeti wa 49 na 50.

49. *Nyumba zao mbake ziwele tame,*
*Makinda ya papo iyu wengeme*
*Husikii hisi wala ukeme;*
*Zitanda matandu walitandaye.*

50. *Madaka ya nyumba za zisahani,*
*Sasa walaliye wana wa nyuni*
*Bumu hukoroma kati nyumbani;*
*Zisiji na koti waikaliye*
*(Al-Inkishafi)*

Umeandikwa na Sayyid Abdallah Nasir na kutafsiriwa na William Hichens (kur. 80-81).

Watumwa walihusika kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza biashara ya mamwinyi kisiwani Pate. Waswahili wa visiwa vya Pate walifanya biashara na kupeleka bidhaa Arabuni na Bara Hindi. Bidhaa hizo zilikuwa ni pamoja na mikoko, magalili ya kasa, kaure, pembe za ndovu na vipusa, meno ya kiboko, ukwaju, magafaa na samagha/gundi. Bidhaa zilizotoka Bara Hindi ni pamoja na nguo, vigae vya kuezeka nyumba, michungi, dhahabu, fedha na dawa za tiba. Bidhaa zilizotoka Uarabuni ni pamoja na tende, utri/mafuta mazuri, papa wakavu, vyetezo na pepeo (Olali, 2023).

Pate pia ilikuwa maarufu kwa sababu ndiko shujaa wa Waswahili Fumo Liyongo alikozaliwa. Pia, kati ya watunzi wa mashairi na tendi za Kiswahili kama vile Mwinyi Aidarusi naye alizaliwa hapa na akatafsiri *Hamziyyah*.

## 5.0 Motifu ya Utumwa Inavyojitokeza katika *Utendi wa Mwanakupona*

Motifu ya utumwa ni kipengele muhimu katika *Utendi wa Mwanakupona*. Mwanakupona anaonesha kuwa uhuru ni haki ya msingi ya binadamu, na kwamba ni lazima kupigania uhuru huo. Anasema kuwa alipigania uhuru wake na hatimaye akapata uhuru huo. Utendi wa Mwanakupona pia unaonesha motifu ya mapambano na ya ukombozi wa kike. Anaeleza kuwa wanawake wanapaswa kuwa na uhuru na haki sawa na wanaume. Anabainisha kwamba wanawake wanapaswa kupigania haki zao na kuishi maisha ya uhuru. Utendi huu ni muhimu kwa sababu mbali na motifu ya utumwa, unaonesha uhuru, mapambano, na ukombozi wa kike. Unaonesha jinsi binadamu wanavyopaswa kupigania uhuru wao na haki zao, na jinsi

wanawake wanavyopaswa kuwa na haki sawa na wanaume. Utendi huu ni muhimu kwa historia ya Kiswahili na kwa mapambano ya wanawake katika jamii ya Waswahili.

**5.1 Ndoa na Upembezwaji wa Mwanamke**

Ndoa ni tukio la mume na mke kula kiapo cha kuishi pamoja hadi kifo kiwatenganishe. Ndoa kama asasi ya jamii imetumika kumdhalilisha mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*. Kwanza, wanaopanga ndoa, huwa ni wazazi na suala la kujichagulia halipewi hadhi. Gibbe (1980) anasema:

> Mwanamke aolewapo hujihisi (na jamii yote hufahamu) kwamba kachukuliwa na mwanamume hufahamu kwamba kachukua. Maisha ya mwanamke hutegemea maisha ya mwanamume. Maisha ya mwanamume kama ni mazuri, ya mwanamke hayani kifani.

Mwanamume na mwanamke wanapaswa kufurahia maisha yao ya ndoa na kukabiliana na changamoto zinazozuka katika ndoa yao. Isichukuliwe kuwa mwanamke ni kifaa tu cha kukidhi uchu wa mwanamume. Asasi ya ndoa husawiriwa kama kigezo cha ukamilisho wa usuhuba. Muungano huu wa mume na mke huwa ni kipaji cha hiari cha pande zote mbili, kwani wao hudhamiria kuanza safari ya kuishi pamoja kama mume na mke.

Desai (1981) anafafanua *nikaah* kama, uthibitisho wa kuafikiana kati ya mume na mke. Upatanisho huu huwaepusha kufanya dhambi na ndio njia kuu ya kulea familia na kundeleza mfumo wa asasi ya ndoa inayosahili, isiyozini na yenye kiunzi cha usafi wa jamii inayodumisha maadili mema.

Sehemu kubwa ya *Utendi wa Mwanakupona* inahusu maandalizi ya Mwana Hashima binti Shee Mataka kwa ajili ya ndoa. Mwanakupona anamfundisha bintiye jinsi ya kuwa mke bora kwa mume wake, akimshauri kuwa na adabu, mtiifu, mwenye upendo, na msaada kwa mumewe. Ubeti wa 13, 26 na 28 ni kielelezo cha jinsi ambayo jamii ya Pate ilimpembeza mwanamke. Pale panapotokea hali ambapo mwanamke anatumiwa kama chombo cha kutawaliwa, huo ni utumwa ambao unaendelezwa ndani ya ndoa.

| | |
|---|---|
| 13. | *Pili uwe na adabu*<br>*Na ulimi wa thawabu*<br>*Uwe mtu mahabubu*<br>*Kula utakapongi* |

Mwanakupona na wanawake wengine wa kipindi chake wanahimizwa wawe na nidhamu na kujizuia kwa namna zozote kuwa katika mstari wa mbele kwenye majibizano ya aina yoyote kila mara. Ule uhuru wa kutoa mawazo hakuna. Mwanamke anashauriwa kumsikiliza tu mumewe. Mshairi anataka mwanamke awe na adabu ndipo aweze kuheshimika na ndiyo hekima yake. Huku ni kudhalilisha

jinsia hiyo na ni utumwa uliomo ndani ya ndoa. Jamii nyingi za Kiafrika ni za kuumeni na Pate haikuachwa nyuma. Tutazame ubeti wa 26.

| | |
|---|---|
| 26. | *Siku ufufuliwao*<br>*Ndhari ni ya mumeo*<br>*Taulizwa atakao*<br>*Ndilo takalotendewa* |

Mwanamke anatekwa kiakili na kuambiwa kwamba itakapofika *Yawm al-Qiyāma* (siku ya kiyama), siku ya kufufuliwa kutoka makaburini, ruhusa ya kukubali afufuliwe itatoka kwa mumewe. Ni siku ya kuwaonjesha wenye dhambi adhabu ya kuungua. Katika ubeti huu, mwanamume ataulizwa kile atakacho, kama mumewe baada ya kufufuliwa, ili atoe idhini ya kile atakachotaka kufanya na mkewe. Huu ni utumwa mkubwa wa kifikra na matilaba yake ni kumdhalilisha mwanamke na kumfanya kama kifaa tu cha kukidhi haja ya mume wake. Kile atakachoulizwa na kujibu basi hicho ndicho kitakachotekelezwa. Ubeti wa 28 unaendeleza upembezwaji huu.

| | |
|---|---|
| 28. | *Keti naye kwa adabu*<br>*Usimtie ghadhabu*<br>*Akinena, simjibu*<br>*Itabidi kunyamaa* |

Katika ubeti huo wa 28, mwanamke anashauriwa kukaa kwa adabu na mume wake. Hata pakitokea jambo gani asijaribu kumfanya mume wake apandwe na hasira. Yeye mwanamke anapaswa kukubali kila kitu anachoambiwa, kiwe kibaya au kizuri. Kiwe sawa au kiwe kimekwenda tirivyogo kama tiara. Mwanamume akisema, mke hapaswi kumjibu hata chembe cha neno. Yeye anapaswa kumsikiliza na kunyamaza kimya. Mwanamke anashauriwa auteke moyo wa mume wake. Kwa hakika, kimya cha mwanamke ni hatari sana katika mahusiano ya ndoa. Mwanamke ni lazima ashirikishwe mambo mbalimbali ya kuijenga ndoa na jamii. Huu ni utumwa wa kimawazo na kifikra. Falsafa inayoongoza hali hii ni ile ya umwinyi ulioshikamana kama gundi na muundo wa jamii za Kiafrika zilizohusudu kuumeni na kumweka mwanamke katika ngazi ya chini.

Katika beti za 60, 43 hadi 46, utendi unatoa maelekezo kuhusu jinsi ya kumtunza mume na familia na jinsi ya kutatua migogoro ya ndoa. Mwanakupona anasisitiza umuhimu wa uvumilivu, heshima na mawasiliano mazuri katika ndoa. Ubeti wa 43:

| | |
|---|---|
| 43. | *Muyuwe alipendalo*<br>*Nawe ufuate lilo*<br>*Yambo limtukialo*<br>*Siwe mwenye kumwetea* |

Mwanamke sharti ajue na kufahamu vizuri yale yote ambayo mume wake anayapenda na anashurutishwa kuyazingatia. Mwanamke anapaswa naye kuvipenda vivyo hivyo avipendavyo mume wake. Hana uhuru wowote wa kusema ni kitu gani akipendacho na asichokipenda. Lazima afuate tu upepo, yaani mume wake. Huu ni utumwa mkubwa. Kama kuna ambacho hakipendi, mwanamke anashauriwa asijaribu kumletea mume wake. Hali hii haiimarishi mahusiano hata kidogo. Itakuwa vigumu hata mume kujua iwapo mkewe anazongwa na huzuni ndani ya nyumba.

Ubeti wa 46 unaonesha namna wanawake wa Kiswahili walivyokuwa wanajivaa. Tukianza na shiraa ambalo pia huitwa ramba, ni vazi la kike kabla ya kuingia kwa buibui au shuga. Shiraa huwa mfano wa hema na hutiwa miti miwili mmoja mbele na mmoja nyuma na wanawake huingia humo. Katikati, kulikuwa na marinda ya kuweza kuingia watu hata ishirini kwa pamoja na kulikuwa pia la mtu mmoja. Shiraa lilikuwa linatumika wakati wanawake walipokuwa wanaenda arusini au matangani. Ubeti huu unamshauri mwanamke kutonena akiwa njiani na kwamba akiwa ndani ya shiraa asiangalie nje na asijioneshe.

| | |
|---|---|
| 46. | *Wala sinene ndiani*<br>*Sifunue shiraani*<br>*Mato angalia tini*<br>*Na uso utie haya* |

Mwanakupona anamshauri Mwana Hashima binti Shee Mataka jinsi ya kumridhisha mume wake na kutimiza wajibu wake wa ndoa; hii ni katika harakati za kutaka ndoa yake isimame thabiti. Hii ni kwenye ubeti wa 26, 27 na 47. Hata siku ya kiyama, itakuwa ruhusa ya mumewe kufanya uamuzi kama tulivyoeleza hapo awali. Lakini ubeti wa 27 unafafanua hali hii zaidi. Kwamba, mume wake ndiye anayefanya uamuzi wa kama yeye (mkewe) anataka kwenda *Jannah*[14]. Akikubali, mara moja hiyo, mkewe ataenda *Jannatul firdaus* na anaongezea kusema kuwa mumewe akisema aende jehanamu, basi hana budi yeye kwenda hukohuko jehanamu. Huu ni utumwa mkubwa wa kisaikolojia.

Utumwa kamili ni kule kutokuwa huru na kusongwa na mambo mengi kama vile makandamizo, vitisho, mateso, kulazimishwa na udanganyifu. Utumwa wa kimapokeo siyo tofauti sana na utumwa wa kisasa. Lakini unapochunguza *Utendi wa Mwanakupona*, unaona taswira ya utumwa mkubwa wa binadamu ambaye anatishiwa kwa kila namna kusudi amtii mumewe. Ni utumwa ambao umejikita katika imani na desturi za kijadi kama inavyodhihirika katika *Utendi wa*

[14] Ingawa hatuambiwi ni *Jannah* ipi. Katika Imani ya Kiislamu kuna *Jannat Al Adan, Jannat Al Firdaws, Jannat An Naeem, Jannat Al Mawa, Dar Ul Khuld, Dar Ul Maqaam na Dar Us Salaam*. Kwa jinsi tunavyoelewa, alikuwa anarejelea *Jannat Firdaws (Jannat Firdaus)* kwa jinsi ambavyo ndiyo ya ngazi ya pili katika *Jannah* na yenye fahari kuu.

*Mwanakupona*. Aina hii ya utumwa inayojitokeza katika *Utendi wa Mwanakupona* ni matokeo ya ubaguzi ambao umekuwa ukiendelea kwa kipindi kirefu sana dhidi ya wanawake na wale ambao walichukuliwa kuwa watu wa matabaka ya chini, kama ilivyokuwa katika kisiwa cha Pate. Utumwa unaoonekana hapa ni ule wa kifikra, kiakili na upembezwaji mkubwa wa mwanamke kama inavyojidhihirika katika beti za 26 na 27.

26. *Siku ufufuliwao*
*Nadhari ni ya mumeo*
*Taulizwa atakao*
*Ndilo takalotendewa*

27. *Kipenda wende peponi*
*Utakwenda dalhini*
*Kinena wende motoni*
*Huna budi utatiwa*

Katika ubeti huo wa 47, Mwanakupona anamshauri bintiye kuwa lazima awe akirudi nyumbani haraka bila kuchelewa. Sababu ya kutakiwa kufanya hivyo ni ili akae na mume wake na kutayarisha mahali pa kulala ili wote wapate usingizi wa pono kama inavyoelezwa katika ubeti wa 47:

47. *Rejea upesi kwako*
*Ukae na mume wako*
*Utengeze matandiko*
*Mupate kuilalia*

**5.2 Dini kama Chombo cha Kumpembeza Mwanamke**

Utumwa unajitokeza kwa upande wa dini vilevile. Dini inajitokeza kwa kiasi kikubwa kwenye *Utendi wa Mwanakupona* hasa kuanzia ubeti wa 67 hadi 102 ambazo zinazungumzia dua yake Mwanakupona kwa bintiye na Waislamu wote kwa ujumla. Kwa hakika, dua yenyewe inawalenga wanawake wapate kulinata shairi hili na wosia uliotolewa. Ni kama dini inatumika kuwadhulumu wanawake. Dini inatumiwa kuendeleza utumwa wa fikra na akili. Inatumika kuwapembeza wanawake.

67. *Kwani yote ninenao*
*Mwanaadamu ni pou*
*Mola ndiye awezao*
*Kupoteza na kongoa*

Hata tukinena kwa njia gani, kwa viwango gani, kwa namna gani, binadamu ni viumbe dhaifu wasio na nguvu ila Mungu ndiye ana uwezo wa kutunusuru au hata

kwa kutuangamiza. Khatib (1985) anasema kwamba *Utendi wa Mwanakupona* ni zao la fasihi ya kimwambao iliyoathiriwa na kupata utomvu wa uhai wake kutokana na utamaduni wa kimwambao uliogoshiwa na maadili ya Kiislamu katika karne ya 19.

Mshairi kabla ya kuanza kumpa mawaidha bintiye, anamwambia cha msingi ni kushika dini na ndio itamwelekeza kufanya yaliyo mema kama anavyosema katika ubeti wa 12:

12. *La kwanda kamata dini*
*Faradhi usiikhini*
*Na sunna ikimkini*
*Ni wajibu kuitia*

Katika ubeti wa 4, Mwanakupona baada ya kumkaribisha bintiye anamwambia apige *bismillahi*[15]. Anaendelea kumwambia kuwa baada ya kulitaja jina la Mola muweza, basi wanaomba ruhusa ya kuendelea na shairi.

4. *Ukisa kutaqarabu*
*Bismillahi kutubu*
*Umsalie Habibu*
*Na sahabaze pamoya*

Anathibitisha kwenye ubeti wa 5 kuwa binadamu si kitu na hakuna mtu ambaye atasalia. Hii inadhihirisha imani ya mshairi na mwanawe kuhusu dini na Mungu kwa kuomba dua kabla ya kufanya chochote kile.
Ubeti wa 5:

5. *Ukisa kulitangaza,*
*Ina la mola muweza,*
*Basi tuombe majaza,*
*Mngu tatufikiya*

6. *Mwana Adamu si kitu,*
*Na ulimwengu si wetu,*
*Walau hakuna mtu*
*Ambao atasaliya.*

*Utenzi wa Mwanakupona* unafundisha maadili ya Kiislamu na umuhimu wa kufuata sheria za dini, ubeti wa 93.

93. *Napenda kumnabihi*

[15] Asili ya neno ni kuwa limefupishwa kutoka kwa *Bismillah-ir-Rahman-ir-Rahim*.

*Laala katanabahi*
*Kamfuata illahi*
*Pamwe na wake rijaa*

Mwanakupona anasisitiza umuhimu wa sala, kufunga, kutoa sadaka na hata kuhiji. Ubeti wa 81 unatoa maelezo kuhusu nguzo tano za Uislamu na jinsi ya kuzitekeleza kwa usahihi. Mwanakupona pia anazungumzia kuhusu sifa za Mungu na umuhimu wa kumwabudu kwa dhati.

81. *Kwa siku hizi tukufu*
*Za kuhiji na kutufu*
*Niafu Rabbi niafu*
*Unishushize afua*

Mwanakupona anawahimiza watu kufuata dini ya Kiislamu na wala si kufuata mambo ya walimu na watu wengine maana kwenye dini ya Kiislamu mtu akiomba hujibiwa. Beti za 75 na 84 zinaeleza kuhusu suala hili.

75. *Wangalie kwa huruma*
*Waongoze ndia njema*
*Uwepulie na tama*
*Za akhira na dunia*

84. *Nipulishie walimu*
*Wakinena yafahamu*
*Dua hini Islamu*
*Akiomba hujibiwa*

Utenzi unawakumbusha wasomaji kuhusu siku ya haki na umuhimu wa kuishi maisha mema yenye kufuata mafundisho ya dini kwenye ubeti wa 88 hadi 90 ambapo anaomba aweze kufika peponi, hivyo, Mungu amwepushie hukumu.

88. *Rabbi unifurahishe*
*Mambo mema unegeshe*
*Maovu uyagurishe*
*Tusikutane pamoya*

Sehemu kubwa ya maudhui katika *Utendi wa Mwanakupona* inasisistiza umuhimu wa kuzingatia mafunzo ya dini ya Kiislamu na kumtii Mungu na vilevile Mtume, kupenda na kutenda haki na kumtii mume (beti 12, 22, 23). Katika ubeti wa 12 anasema ;
Ubeti wa 12:

12. *La kwanda kamata dini*
*Faradhi usiikhini*
*Na sunna ikimkini*
*Ni wajibu kuitia*

22. *Mama pulika maneno*
*Kiumbe ni radhi tano*
*Ndipo apate usono*
*Wa akhera na dunia*

23. *Nda Mngu na Mtumewe*
*Baba na mama wayuwe*
*Na ya tano nda mumewe*
*Mno imekaririwa*

Kwa kweli, dini inapinga utumwa ambao ulimfanya mwanamke aonekane kama kijakazi na asiweze kushiriki katika shughuli za kijamii. Mwanamke ana uwezo katika kutenda kazi na kupigana na ubabedume. Uislamu, kwa hakika, umeweka kanuni kamili kuhusu yule anayemmiliki mtumwa na endapo atamdhuru kwa njia yoyote ile; basi, anapaswa kumwachilia huru na wala siyo hiari. Mwanakupona anarejelea dini kwa kumshauri bint Shee Mataka, binti yake, kuhusu tabia njema anayotakiwa kuwa nayo kama mwanamke. Hii inajumuisha kuwa mtiifu kwa mumewe, wazazi wake, kuwa mkarimu kwa watu wote, na kujiheshimu kwenye beti za 11, 13 na 21.

11. *Yangu utakaposhika*
*Mwanangu hutosumbuka*
*Duniani utavuka*
*Na akhira utakia*

Katika ubeti huu wa 11, Mwanakupona anamshauri binti yake kumtii mumewe na kusikiliza yote anayoyasema, hivyo, kusumbuka. Utumwa wa kifikra na kiakili unajitokeza hapa ambapo anashauriwa kuwa asipofanya hivyo, hataweza kupata pingamizi au vikwazo vyovyote duniani. Akifanya hivyo, ataenda ahera.

13. *Pili uwe na adabu*
*Na ulimi wa thawabu*
*Uwe mtu mahabubu*
*Kula utakapongiya*

Dini imekuwa ikitumika kama chombo cha kumpembeza mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika, hasa katika tamaduni za Kiswahili. Katika dini za Kiafrika, mwanamke anaonekana kama kiumbe mwenye thamani kubwa. Dini inamwona

mwanamke kama mama, mke na dada, na kumheshimu kwa nafasi yake katika jamii. Katika dini ya Kiislamu, mwanamke ana nafasi ya heshima kubwa. Kurani inaeleza kuwa mwanamke na mwanamume wameumbwa kwa usawa na kwamba wana heshima sawa mbele ya Mungu. Mwanamke ana haki ya kupata elimu, mali na uhuru wa kuchagua maisha yake. Katika tamaduni za Kiafrika, mwanamke anaonekana kama msimamizi wa familia na anaheshimiwa kwa nafasi yake. Mwanamke ana haki ya kupata elimu, mali na uhuru wa kuchagua maisha yake. Katika baadhi ya tamaduni, mwanamke anaonekana kama kiongozi wa jamii na anaheshimiwa kwa uongozi wake.

### 5.3 Watumwa Wakirejelewa kama Wajinga

Awali tuliona matabaka mbalimbali katika kisiwa cha Pate huku ukoo wa Nabahani wakiwa katika ngazi ya juu zaidi na ile ya Wapate ama Waswahili wakiwa katika ngazi ya chini. Utabaka ulikuwapo kisiwani Pate. Utabaka ni hali inayojitokeza katika jamii ambapo watu hujigawa kulingana na mali waliyo nayo, elimu, madaraka kazini ama imani za dini. Kati ya matabaka mengi yanayoshuhudiwa katika jamii, tabaka la walalaheri na walalahoi ndilo linaloshamiri zaidi.

Katika mfumo wa Kimwinyi, kuna tabaka tawala na tawaliwa (wenye nacho na wasionacho). Mwanakupona alikuwa katika tabaka tawala, na hili tunaliona katika beti za 20 na 21 anapomwasa binti yake kutochangamana na watumwa na wajinga walio katika tabaka la chini.

| | |
|---|---|
| 20. | *Sitangane na watumwa,*<br>*Ila mwida wa khuduma,*<br>*Watakuvutia tama,*<br>*La buda nimekwambiya.* |

Anamshauri bintiye kutotangamana na watumwa maana watamkatisha tamaa na kumfanya kuwa maskini. Tunapata taswira ya kuwa mtunzi alikuwa wa tabaka la juu na kuwa kulikuwa na ubaguzi wa kitabaka enzi hizo. Ubeti wa 21 unadhihirisha haya.

| | |
|---|---|
| 21 | *Sandamane na wainga*<br>*Wasoyua kuitunga*<br>*Ziumbe wasio tanga*<br>*Wata kuwaqurubia* |

Katika ubeti wa 21 anamshauri binti yake, kwa vyovyote vile, kuwaepuka watu wote ambao hawaelewi jinsi mambo yanavyoendeshwa au kupangwa katika jamii, ambao anawaita wajinga. Ubeti huu unadhihirisha utabaka ulivyokuwa dhahiri. Wengine walichukuliwa kama wajinga ambao hawastahili kuheshimiwa. Ni wajinga ambao wana utovu mkubwa wa uungwana, sifa kubwa miongoni mwa mamwinyi wa Pate. Anakatazwa kutangamana nao kwa sababu ni watu waliokosa cha kufanya, viumbe

hafifu. Bila shaka, ubeti huu unaonesha watu wa daraja la chini kabisa kama watumwa, vijakazi, yaani watu wa matabaka ya chini kabisa.

Katika hali hii, anapoonywa kuhusu kutangamana na wajinga, anashauriwa jinsi ya kuishi na mwanamume. Watumwa waliorejelewa kama wajinga na hawakupaswa kutangamana naye. Badala yake, Mwanakupona anatenga beti kadhaa za kumshauri mwanawe jinsi ya kuishi na mumewe. Utenzi unatoa maelekezo ya kina kuhusu jinsi ya kusimamia kaya, ikijumuisha jinsi ya kupika, kusafisha na kutunza watoto. Mwanakupona anasisitiza umuhimu wa kuwa mchapakazi na msafi na kuwa na ujuzi mzuri wa usimamizi wa nyumba. Hayo yanabainika katika beti za 33, 34, 37, 39 na 42 (ni ushauri huo).

33. *Chamka simuhuli*
*Mwandikie maakuli*
*Na kumtunda muili*
*Kumsinga na kumwoa*

Utumwa wa kiakili na fikra unajitokeza katika ubeti huu wa 33 ambapo mwanamke anachukuliwa kama kifaa ama chombo cha kumlisha na kumsinga mumewe. Kwamba anapoamka tu, mwanamke anashauriwa kutocheleweshа chakula chake na aandaliwe vizuri na kuwekewa mbele yake. Mwanamke wa Kiswahili atamwandalia mumewe vyakula kama vile alu[16], bakalawi[17], bodo[18] na matobosha[19]. Isitoshe, anapaswa kumsinga mwili[20], kumfukizia manukato na kumwosha.

34. *Mnyoe mpalilize*
*Sharafa umtengeneze*
*Na udi umfukize*
*Bukurata wa ashia*

[16] Viazi vya mviringo ambavyo hupikwa pamoja na nyama mpaka ikanywea katika maji yatokayo katika nyama au rigiyaani (supu).

[17] Aina ya keki au chapati ambayo hutiwa lozo, sukari, na zabibu na zote hizo lazima ziwe kipimo chake sawasawa.

[18] Chakula ambacho hupikwa kwa unga wa mahindi kwa Kitikuu. Utaiti kwa Kiamu, na sima Kimvita. Vilevile, chakula hiki kikipikwa katika jahazi kwa Kiamu huitwa sende.

[19] Aina ya chakula cha unga wa ngano kinachotiwa tamu ya sukari na hufanywa vidogovidogo na kufanywa vishimo. Umbo lake ni kama kunazi.

[20] Kusinga mwili husaidia kuondoa uchafu mwilini, kufubaa kwa ngozi na pia kupunguza maumivu ya mwili na kumfanya anayesingwa kupata pumziko na kupunguza msongo wa mawazo.

Mwanakupona anamuusia bintiye kuwa anapaswa kumnyoa mumewe kichwa, sharafa zake kidevuni, na amfukizie udi[21], usiku na mchana. Mwanamke ni kama chombo tu cha kumfurahisha bwanake.

| | |
|---|---|
| 37. | *Mwanangu siwe mkoo*<br>*Tenda kama uonao*<br>*Kupea na kosha choo*<br>*Sidharau mara moya* |

Anaambiwa amwangalie mumewe kama mtoto mchanga ambaye hajajua kuzungumza na hasa upande wa kile kinachoingia mwilini mwake.

| | |
|---|---|
| 39. | *Nawe ipambe libasi*<br>*Ukae kama arusi*<br>*Maguu tia kugesi*<br>*Na mikononi makoa* |

Mwanamke anashauriwa kujipamba na kujiweka nadhifu kabisa kama bibi arusi na kuvalia kugesi[22] vilevile bangili[23]. Kisiwani Pate, wanawake pia walipaswa kuvalia vipini[24], vipuli[25], vipeperenge[26], mashahasi[27] na peto[28].

| | |
|---|---|
| 42. | *Nyumba yako i nadhifu*<br>*Mumeo umsharifu*<br>*Wakutanapo sufufu*<br>*Msifu na kumtaya* |

[21] Hivi ni vipande vya mti maalumu ambao una harufu nzuri sana ukiutia katika moto na watu hujifukizia na pia Waswahili huchukua unga wa miti ambayo imepatikana na kuupika kwa mafuta mazuri na kupikwa kwa sukari. Wanawake wa Kiswahili wanapenda sana kujifukiza wao na nguo zao pamoja na mabuibui au mashuga.

[22] Pia, vinaitwa vikuku au furungu.

[23] Katika kisiwa cha Pate, bangili walizozivaa wanawake zilikuwa za ng'andu au dhahabu na zinavaliwa mkononi kama kikuku. Kinavaliwa juu ya kiwiko.

[24] Chombo cha ng'andu au dhahabu kinachovaliwa puani katika tundu lililotobolewa upande wa kulia juu ya pua.

[25] Chombo cha dhahabu kinachovaliwa katika ncha ya ndewe sikioni.

[26] Aina ya kipuli ambacho huvaliwa juu ya ndewe katika pambizo za masikio.

[27] Chombo cha dhahabu kilicho mviringo na kinachovaliwa puani upande wa kushoto kama kipini.

[28] Mkufu unaovaliwa shingoni. Huwa ni wa dhahabu au fedha.

Nyumba lazima isafishwe ili kumfurahisha mume. Huu ni utumwa wa kifikra na wa kiakili. Kwamba watu wanapoitembelea nyumba ile, wanakuwana furaha na vilevile huzungumza mazuri yote kumhusu mumewe.

Kulingana na Bank (1986), nyuso za mwanamke ni mikakati tofautitofauti inayochukuliwa na wafeministi mbalimbali ili kupigania haki na usawa wa mwanamke. Mathalani, katika karne ya 18, vitengo vitatu vya kiusomi vilijitokeza na kila kitengo kiliwa na harakati tofauti za kupigania haki na usawa wa mwanamke.

Usafi wa mwanamke unasisitizwa sana kwenye utendi huu. Utendi unafunza kuhusu umuhimu wa usafi nyumbani kama tusomavyo katika beti za 37 na 42. Anasema:

37. *Mwanangu siwe mko'o*
*Tenda kama uona'o*
*Kupea na kuosha choo*
*Sidharau mara moya.*

42. *Nyumba yako inadhifu*
*Mumeo umsharifu*
*Wakutanapo sufufu*
*Msifu ukimweteya*

Baadhi ya wahakiki wa utendi huu wamesema kuwa beti hizi zinamuasa mwanamke ajirembe na kujipamba. Beti za 37 na 42 zinasisitiza kuhusu umuhimu wa usafi wa mwili zaidi ya kujipamba tu. Ili kuweza kutoa tafsiri ya beti hizo labda itambidi msomaji binafsi aamue mwenyewe. Ila ni wazi kwamba usafi uliotajwa pamoja na urembo na kujipamba kunakosisitizwa katika beti hizo - vyote hivi vimeelekezwa katika kumpendeza na kumfurahisha mwanamume kuliko kuwa na manufaa kwa mwanamke mwenyewe. Utenzi huu kwa mujibu wa Senkoro unaendeleza umwinyi. Huu unajitokeza wakati Mwanakupona anamtaka binti yake ajipambe na kuendana na mfumo wa kimwinyi, kwa sababu anatilia maanani yale mambo ambayo yanawavutia wanaume. Katika ubeti wa 39 anasema:

*Nawe jipambe libasi*
*Ukae kama arusi*
*Maguu tia kugesi*
*Na mikononi makoa*

Huu ni utumwa kwa sababu mwanamke anaonekana kama pambo tu. Suala hili ni la muhimu sana katika jamii zetu kwani katika kujishughulisha ndipo tunapoweza kujikomboa kutoka katika utumwa na utegemezi wa ndugu na jamaa zetu. Kwa mtazamo wa jamii, mwanamke ni kiumbe anayehusishwa na kazi za nyumbani na pia malezi ya watoto na huku akielekezwa na jamii kuzingatia utamaduni huo.

Ingawa kwa sasa kuna mwamko mpya wa kushirikiana nyumbani kwa kazi kati ya mwanamke na mumewe, mwanamke angali anafanya kazi nyingi.

Mshairi anasisitiza kuwajibika kama mwanamke kwa kupika, kuosha vyombo na usafi kwa jumla na kuilinda ndoa yake ipasavyo. Bbeti za 49 na 59 ni mifano mizuri ya jinsi mwanamke anavyodhalilishwa katika kisiwa cha Pate.

49. *Akupacho mpokee*
*Na moyo ufurahie*
*Asolitenda kwa yeye*
*Huna haja kumwambia*

Katika mfano uliotolewa katika ubeti wa 49 hapo juu, ni wazi kuwa utendi huu haukuwa tu kwa ajili ya bintiye bali pia utendi wanawake wengine wa Kiswahili. Mfano huu unamshauri mwanamke kupokea chochote atakachopewa na mumewe akipokee kwa furaha. Pale mwanamume afanyapo kitu ambacho mwenyewe hakukitarajia, mwanamke anatakiwa kukaa kimya.

59. *Na wachandika chakula*
*Uchambiwa nawe nia*
*Wala siweke muhula*
*Nyumanyuma kurejea*

Ubeti huu una maana nzito. Unaonesha kuwa chakula kinachotolewa kwa mtu kinapaswa kuwa na nia njema. Hii ina maana kuwa mtu anayekulisha anapaswa kuwa na nia ya dhati ya kukupenda na kukusaidia. Mtu hapaswi kuwa na nia mbaya au ya kulipiza kisasi. Anapaswa kuwa na moyo safi na asikumbuke mabaya yaliyopita.

Anamshauri bintiye kuwajibika kwa kuwa msafi na kujipamba ili kumpendeza mumwewe. Hilo linajidhihirisha katika beti za 38, 39, 40 na 41.

38. *Na kowa na kuisinga*
*Na nyee zako kufunga*
*Na asmini kutunga*
*Na firashani kutia*

39. *Nawe ipambe libasi*
*Ukae kama arusi*
*Maguu tia kugesi*
*Na mikononi makoa*

40. *Na kidani na kifungo*
*Sitoe katika shingo*
*Muili siwate mwingo*
*Kwa marashi na dalia*

41. *Pete sikose zandani*
*Hina sikome nyaani*
*Wanda sitoe matoni*
*Na nshini kuitia*

Malezi ni hali ya kuelekezwa na kupata mafundisho kwa mujibu wa sera za jamii. Malezi tunayokumbana nayo ni yale yanayomkandamiza mwanamke. Utendi mzima ni zao la malezi mema maana Mwanakupona anawajibika kama mzazi kwa kumpa maelekezo mwanawe jinsi ya kushika dini, jinsi ya kumlinda mumewe na maadili kwa ujumla kwa kumwambia yale maovu ambayo anastahili kuepukana nayo na mazuri ambayo anatakiwa kuyafanya. Inaonekana ni vigumu kutoa madai kuwa huu siyo utumwa wa fikra. Kwa mujibu wa Mwanakupona, mwanamke ana jukumu la kutoa malezi kama mzazi. Mwanakupona anachukua muda wake kuwausia wasichana wote mbali na bintiye jinsi ya kumlinda mume na ndoa kwa ujumla. Hata hivyo, kile kinachodhihirika ni utovu wa heshima kwa mwanamke. Katika beti za 58, 59, 60 na 66, tunaona hali hii ya kumteka mwanawe akili na kumpa masharti ya kutekeleza.

58. *Uwaonapo swahibu*
*Ambao wakunaswibu*
*Akwambiapo qaribu*
*Angusa kuqurubia*

59. *Na wachandika chakula*
*Uchambiwa nawe nia*
*Wala siweke muhula*
*Nyumanyuma kurejea*

60. *Wala sifanye kiburi*
*Nia hata ushakiri*
*Usiyakuta siqiri*
*Ukamba ni kondolewa*

66. *Tamati maneno yangu*
*Kukuusia mwanangu*
*Sasa ntamuomba Mngu*
*Anipokelee dua*

Mwanakupona anatanguliza wosia wake kwa kumwombea bintiye kwa Mola ili amhifadhi na kumwondolea baa kwenye ubeti wa 7. Hii inadhihirisha changamoto za maafa na baa ambazo zinamwandama binadamu katika maisha ya kila siku. Kimsingi, kuna kudhalilishwa kwa mtoto wa kike.

7. *Mwanangu twaa waadhi*
*Pamoya na yangu radhi*
*Mngu atakuhifadhi*
*Akuepue na baa*

Mshairi anamshauri bintiye kuepukana na wasaliti ambao watamsababishia maovu siku zote kwenye ubeti wa 61. Hii inadhihirisha uovu ambao upo.

61. *Watu wote waumini*
*Kwako na wawe wendani*
*Sipende masalatini*
*Washinde ukiwepua*

Mshairi anawaombea wote Mola awaongoze njia njema, awaepushie na tamaa za akhira na dunia, ubeti wa 75. Hizi ni baadhi ya changamoto ambazo watu wanapitia kila siku.

75. *Wangalie kwa huruma*
*Waongoze ndia njema*
*Uwepulie na tama*
*Za akhira na dunia*

Mwanamke amechorwa kwa namna tofautitofauti kutokana na mjadala uliozua mitazamo tofauti kuhusu utenzi huu. Tukiangalia tapo linaloona kuwa utendi huu unamdhalilisha mwanamke, tunaona mwanamke anachorwa kama kiumbe duni na dhaifu na kwamba anatakiwa kumtegemea mumewe kwa kila kitu na kumtii. Katika ubeti wa 28 anasema:

*Keti naye kwa adabu*
*Usimtie ghadhabu*
*Akinena simjibu*
*Itahidi kunyamaa*

Pia, tunaweza kuona kuwa mwanamke amechorwa kama mlezi. Mwanakupona katika kumlea binti yake anatunga utungo huu ili umsaidie kulinda ndoa, si yeye tu bali na mabinti wengine wa Kiafrika. Katika ubeti wa 9 mshororo wa kwanza anamwambia binti yake 'nikutungie kindani'.

9. *Nikutungie kindani*
*Cha lulu na marijani*
*Nikuvike mke shani*
*Shingoni kikizagaa*

Pia, katika ubeti wa 92 anasema:

*Na sababu ya kutunga,*
*Si shairi si malenga,*
*Nina kijana muinga,*
*Napenda kumuusia*

Mwanamume amechorwa kama mwenye mamlaka na madaraka katika jamii. Jamii nyingi za Kiafrika ni za kuumeni. Anaonekana kummiliki mwanamke na ndiyo maana hata siku ya kiyama itakapofika, ndiye mwenye uamuzi juu ya mke wake kwamba aende motoni au peponi. Tunaona hili katika beti za 26 na 27. Mtunzi anasema:

*26.* *Siku ufufuliwao*
*Nadhari ni ya mumeo*
*Taulizwa atakao*
*Ndilo takalotendewa*

*27.* *Kipenda wende peponi*
*Utakwenda dalhini*
*Kinena wende motoni*
*Huna budi utatiwa*

Mshairi anamuasa binti yake kuepuka tabia ya uvivu na uzembe, na anamtaka kuonyesha bidii na juhudi katika kazi, na hasa pindi awapo na mumewe. Katika ubeti wa 37 anasema:

*Mwanangu siwe mkoo*
*Tenda kama uonao*
*Kupea na kosha choo*
*Sidharau mara moya*

Jinsi suala hili linavyojitiokeza linaonyesha kutekwa kiakili na kifikra, ni namna fulani ya utumwa. Haya yanajitokeza pale Mwanakupona alipotoa maadili mbalimbali kwa binti yake, kwa mfano, katika beti za 11, 12, 13, 14 na 15 anasema:

11. *Yangu utakaposhika*
*Mwanangu hutosumbuka*
*Duniani utavuka*
*Na akhira utakia*

12. *La kwanda kamata dini*
*faradhi usiikhini*
*Na sunna ikimkini*

*Ni wajibu kuitia*

13. *Pili uwe na adabu*
*Na ulimi wa thawabu*
*Uwe mtu mahabubu*
*Kula utakapongia.*

Hapa, anamtaka binti yake awe na heshima na kutumia ulimi wake vizuri pale anapokuwa na watu, na kwa njia hiyo atajijengea heshima kwa watu wote kama anavyobainisha katika ubeti wa 14.

*La tatu uwe sadiqi*
*Wambiwao ulithiqi*
*Mtu asoshika haqi*
*Sandamane naye ndia.*

Anaongezea kusema katika ubeti wa 15:

*Tena mwanangu idhili*
*Mbee za maqabaili*
*Uwaonapo mahali*
*Angusa kuwenukia*

Mila, desturi na jadi ya Waswahili/Waafrika imechangia kwa kiasi kikubwa kuleta utumwa wa namna hii. Wanajamii huwa na mambo mbalimbali wanayoamini na hujaribu kuyafuatilia huku wakisadiki kwamba imani zao hufaulu. Matokeo ya kufaulu huwa na mikakati ya kukabiliana nayo.

Mathalani, Waafrika wanazo mila na desturi za jadi kuhusu mahusiano ya watu katika ndoa na maisha kwa ujumla ambazo huwafundisha watoto wao. Mafunzo hayo kijadi yalikuwa yakitolewa katika unyago, ngano na masimulizi mengine na katika matendo ya kimila ya kila siku. Adabu na heshima, kuepuka umbea na fitina, kujiheshimu, kupenda kazi, uzazi na kuishi ndani ya nyumba bila vikwazo ni baadhi ya mambo yaliyofungamana na utamaduni wa Waswahili. Mtunzi anataka mwanawe aishi vyema na watu wote kwa kushirikiana na wanandugu, marafiki, na watu wengine. Pia, anatakiwa awasaidie wale wenye uhitaji wa msaada kwake.

## 6.0 Hitimisho

Mtazamo ambao tumeuchukua katika kuandika makala hii huenda ukazua mijadala mikali. Mijadala hiyo inaweza ikawa baina ya wale wenye kuishika dini ya Kiislamu na wasomi ambao wanaangalia utumwa wa kisasa katika misingi ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Hata tunapoangalia utumwa wa kisasa, ni dhahiri kuwa utumwa uliendelea katika kisiwa cha Pate na funguvisiwa vya Lamu na kwamba

tunapata hali hii katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Utendi huu ni wa kale na maarufu sana. Licha ya ukale wake, utenzi huu ni nguzo muhimu katika kuelekeza kizazi cha awali na hata kizazi cha sasa kwenye masuala mbalimbali ya kijamii kama vile utumwa wa kiakili, wa kifikra na upembezwaji wa jinsia ya kike pamoja na utabaka. Ingawa ni utenzi unaoelekeza njia salama za kidini, msimamo wetu ni kwamba dini inatumika kuwadhulumu wanawake haki zao.

*Utenzi wa Mwanakupona* unachangia kama sehemu mojawapo ya kupata historia ya utumwa katika upwa wa Afrika Mashariki na jinsi ambavyo watu waliishi kisiwani Pate kitabaka. Hii ni sehemu muhimu ya historia ya mamwinyi, masultani, masultana pamoja na mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki. Elimu ya utumwa bado ni adimu kuipata kikamilifu katika fasihi ya Kiswahili. *Utendi wa Mwanakupona* ni kati ya tendi za Kiswahili ambazo zinachangia uwanja huu wa utumwa. Ni mchango wa fasihi katika kuiangalia mada ya utumwa. Kwa mintarafu hii, *Utendi wa Mwanakupona* ni tarihi ya kihistoria inayotoa habari kuhusu utumwa katika kisiwa cha Pate.

## Marejeleo


Beja, S. na Mwinyifaki, A. (2013). 'Iktibasi' katika *Tenzi za Mwanakuponana* na *Al-Inkishafi*. *Kioo cha Lugha*. 11(1): 30-46.

Bank, O. (1990). *Faces of Feminism: A Study of Feminism as a Social Movement*. Oxford: Basil Blackwell.

Biersteker, A. (1991). "Language, Poetry and Power: A Reconstruction of 'Utendi wa Mwana Kupona.' Katika K.W. Harrow (Mh.), *Faces of Islam in African Literature*. London: James Currey. Kur. 37-58.

Desai, S. (1998). *Ta' Lemul Haq Ne*. Delhi: Millat Book Centre.

Frederick, C. (1977). *Plantation Slavery on the East Coast of Africa*. New Haven and London: Yale University Press.

Ghaidan, U. (1975). *Lamu: A Study of a Coastal Town*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Gibbe, A. (1980). *Shaaban Robert: Mshairi*. Da es Salaam: Tanzania Publishing House.

Gibbe, A. (1995). Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Moi. Eldoret.

Grenville, F. (1988). *The Swahili Coast, 2nd to 19th Centuries*.London: Variorum Reprints Publishers.

Kiriama, H. (2018). "The Landscapes of Slavery in Kenya". *Journal of African Diaspora*
*Archaeology and Heritage*. 7(2):192-206.

Hichens, W. (1972). *Al-Inkishafi, The Soul's Awakening*. Nairobi: Oxford University Press.

Khatib, M. (1985). "Utenzi wa Mwana Kupona". *Mulika*. 17: 46-52.

Mdee, J., Njogu, K na Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Mkufya, M. (2007). *Utenzi wa Mwanakupona Binti Mshamu*. Nairobi: JKF.

Momanyi, C. (2007). “Patriachal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuated in Waswahili Poetry”. *Journal of Pan African* Studies. 1 (8): 12-21.

Mulokozi, M. (1989). *‘Tanzu za Fasihi Simulizi’* katika *Mulika*. Juzuu, 21 kur. 1-24.

Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Munyole, S.D. (2017). Usomaji na Ufasiri Sasa wa Utenzi wa Mwana Kupona. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta

Nasasira, J. (2023). *Muhtasari wa Mwanakupona*. Kampala: Researchgate Inc.

Ngunjiri, D. (2012). Matumizi ya Taswira kama Kigezo cha Kufanikisha Maudhui katika Utendi wa Siiraji uliyotungwa na Muhammadi Kijumwa. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njozi, H. (1990). *Utendi wa Mwana Kupona* and Reception Aesthetics. *Kiswahili*. 57: 55-67.

Nwulia, M. (1975). *The East African Slave Trade-Britain & Slavery in East Africa*.

Washington DC: Three Continents Press.

Olali, T. (2004). The Veneration of the Prophet: The Role of Kasida ya Hamziyyah During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha London.

Olali, T. (2012). *Performing Arts in Lamu*.London: Lambert Academic Publishing.

Olali, T. (2023). Trying the Sails from the Lamu Archipelago to the Arabian Gulf: The death’ of *Mtepe* and Subsequent Rise of Jahazi. *Kiswahili*. 86(1): 89-104.

Prins, J. (1961). *The Swahili-Speaking Peoples of Zanzibar and the East African Coast*. London: International African Institute.

Radburn, N. (2016). The Long Middle Passage: The Enslavement of Africans and the Transla-Atlantic Slave Trade, 1640-1808. Baltimore: John Hopkins University Press.

Rockel, S. (2025). “The 19th Century Slave Trade in Eastern Africa.” https://doi.org/10.1093/acrefore/9780190277734.013.598

Senkoro, F. (1988). *Ushairi; Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Inter Press of Tanzania Limited.

Strobel, M. (1979). *Muslim Women in Mombasa. 1890-1975*. New Haven and London: Yale University Press.

Taiwo, O. (1984). *Female Novelist of Modern Africa*. Lagos: Macmillan Publisher.

Timammy, R. na Swaleh, A. (2013). “A Thematic Analysis of Utendi wa Mwana Kupona: A Swahili Islamic Perspective”. *Journal of Education and Practice*. 4 (28): 8-15.

Tolmacheva, M. (1993). *The Pate Chronicle.* New Haven: Michigan State University Press.

Wandera, S. (1996). *Usawiri wa Mwana Kupona katika Ushairi wa Kiswahili: 1800-1900; Uhalisi au Ugandamizwaji?* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of Women*. Harmondworth Penguin: Blackwell Publisher.

Ylvisaker, M. (1975). *The Political and Economic Relationship of the Lamu Archipelago to the Adjacent Kenyan Coast in the Nineteenth Century.* Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Boston.